TANGAZO LA SERIKALI NA.150 la tarehe 3/3/2023

SHERIA YA MIPANGO MIJI

(SURA 355)

# AMRI

*(Imetengenezwa Chini ya Kifungu cha 8(1) na 23(1))*

AMRI YA KURASIMISHA MAKAZI YASIYOPANGWA ENEO LA ILOLO YA MWAKA, 2023.

Jina:

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Kurasimisha Makazi Yasiyopangwa Eneo la Ilolo ya mwaka, 2023

Utangazaji wa Eneo la Upangaji Sura (355)

2. Eneo lililoainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa eneo la upangaji (mpango wa urasimishaji) kwa madhumuni ya Sheria ya Mipango Miji

Mpango katika eneo la kwenye Jedwali

3. Mipango ya jumla na kina ya eneo lililoainishwa katika Jedwali itaandaliwa na kuhifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Mipango Miji na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa.

JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

Eneo la urasimishaji lipo ndani ya mipaka ifuatavyo:-

"Unaanzia kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba IL1 yenye majira - nukta 220598MS, 9296338KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Mashariki katika uelekeo wa KZ $31^0$01'97''MS kwa umbali wa kilometa 0.72 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba IL2 yenye majira - nukta 220598.00 MS ,9296338.00 KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini – Mashariki kwa kufuata barabara ya Magereza katika uelekeo wa KS $60^0$58'31.73''MS kwa umbali wa kilometa 0.74 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba IL3 yenye majira - nukta 221245.00 MS, 9295979.45KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini - Magharibi katika uelekeo wa KS$46^0$16'46.99''MG kwa umbali wa kilometa 0.53 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba IL4 yenye majira - nukta 220856.144MS; 9295607.607 KZ, baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Magharibi katika uelekeo wa KZ$52^0$19'35.06''MG kwa umbali wa kilometa 0.199 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba IL4 yenye majira - nukta 220698 MS,

9295729 KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini - Magharibi kwa kufuata barabara ya Kibakwe katika uelekeo wa KS $44^0$ 42'43.50''MG kwa umbali wa kilometa 0.56 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba IL5 yenye majira - nukta 220302MS, 9295329 KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Mashariki katika uelekeo wa KZ $11^0$ 11'47.72''MS kwa umbali wa kilometa 0.39 hadi ulipoanzia."

Dodoma,
6 Februari, 2023

ANGELINE S. MABULA,
*Waziri wa Ardhi, Nyumba na,*
*Maendeleo ya Makazi*